## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA NNE 2016/2017) ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA TAREHE 30/07/2017.

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

1. Mhe. Chitwanga R. Ndembo - Diwani Mtunguru - Mwenyekiti
2. Mhe.Rashid Akbar Mbunge - Mjumbe
3. Mhe. Swalehe .F. Amri - Diwani Chitekete - Mjumbe
4. Mhe. Saleh K.Milanzi - Diwani Mpwapwa - Mjumbe
5. Mhe. Rashidi B. Songoni - Diwani Chihangu - Mjumbe
6. Mhe. Shaibu R. Ngumbe - Diwani Kitangari - Mjumbe
7. Mhe. Zaituni L. Nawanda - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
8. Mhe. Mohamed A. Mnyolokoto-Diwani Muungano - Mjumbe
9. Mhe. Zainabu R. Mpita - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
10. Mhe. Rashidi Nambomo - Diwani Mnyeu - Mjumbe
11. Mhe. Bakari C. Mniyopa - Diwani Malatu - Mjumbe
12. Mhe. Fabian J. Mahanyuka - Diwani Mnyambe - Mjumbe
13. Mhe. Saidi Y. Mawangwa - Diwani Makukwe - Mjumbe
14. Mhe. Hadija M. Likwembe - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
15. Mhe. Rashidi H. Lugomba - Diwani Nakahako - Mjumbe
16. Mhe. Selemani A. Mtili - Diwani Mkwedu - Mjumbe
17. Mhe. Raia R. Nang'oko - Diwani Mikumbi - Mjumbe
18. Mhe. Selemani M. Hiyari - Diwani Mkoma II - Mjumbe
19. Mhe. Sauda R. Rashidi - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
20. Mhe. Zakina A. Mduma - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
21. Mhe. Maua Makubui - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
22. Mhe. Yahaya A. Lisinge - Diwani Nandwahi - Mjumbe
23. Mhe. Hashimu B. Namawa - Diwani M/ Mpelepele - Mjumbe
24. Mhe. Arabia H. Mkwatile - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
25. Mhe. Amina Mkanangwamba - Diwani Viti Maalum - Mjumbe
26. Mhe. Jamali J. Nandonde - Diwani Chilangala - Mjumbe
27. Mhe. Hanafi N. Nahonyo - Diwani Mtopwa - Mjumbe
28. Mhe. Athumani M. Mniwasa - Diwani Chiwonga - Mjumbe
29. Mhe. Simon F. Nachingulu - Diwani Nam-bali - Mjumbe
30. Mhe. Munga Mohamedi - Diwani Mchemo - Mjumbe.
31. Mhe.Menas M.Likuku -Diwani Maputi - Mjumbe

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA:** Hakuna

**WATAALAMU/WASHAURI**

1. Ndg. Mussa M.Chimae - Mkurugenzi Mtendaji(W)-Katibu
2. Ndg. Shakira Ahmad - Afisa Utumishi na Utawala (W)
3. Ndg Shada L.Nankoko - Kaimu Afisa Utamaduni
4. Ndg. Tumaini .S. Abdallah - Afisa Biashara
5. Ndg. Nsajigwa Mwakatika - Kaimu Katibu TSC (W)
6. Ndg. Omary Msuya - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
7. Ndg. Evance Lusuva - Kaimu Mthibiti na Mkaguzi Ubora wa Shule
8. Ndg. Joseline Chambasi - Afisa Habari
9. Ndg. Wilson Mafumba - Mkaguzi wa Ndani
10. Ndg. Alford Mpanda - Afisa Kilimo,Ushirika na Umwagiliaji (W)
11. Ndg. Msafiri Ngai - Kaimu Afisa Ugavi (W)
12. Ndg. Christina Kambuga - Afisa Maendeleo ya jamii(W)
13. Ndg. Famili Mshaghira - Afisa Utumishi
14. Ndg. Mahundu Innocent - Afisa Ushirika
15. Ndg.Macha Benjamini - Kaimu Afisa Usafirishaji
16. Ndg. Benaya Sanane - Mchumi
17. Ndg Rogers Muganyizi - Afisa Ardhi(W
18. Eng. Nsajigwa Sadiki - Mhandisi Maji (W)
19. Eng. Sylvester Balama - Mhandisi Ujenzi (W)
20. Ndg. Magreth Likonda - Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira (W)
21. Ndg. Shabani .K. Maganga - Kaimu Mganga Mkuu (W)
22. Ndg. Hassan Mtamba - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)
22.Ndg. Prosper Haule - Meneja wa Redio Newala FM
23.Ndg. Lucy Matem - Afisa Sheria
24.Ndg. Marry Chilemba - K/ Afisa Afya na Mazingira
25. Ndg. Juma .I. Rahisi - Kaimu Afisa Mipango (W)
26. Ndg. Nuru Ringo - Kaimu RAS-Mtwara
27. Ndg. Majidu Kalugendo - Afisa Elimu Sekondari (W)
28. Ndg. Julius .B. Kiyanga - Kaimu Afisa Tarafa Mkwedu
29. Ndg. Mshamu Y.S. - Kaimu Afisa Tarafa Chilangala
30. Ndg. Agnes .L. Mnipalika - Mtendaji Kata Mchemo
31. Ndg. Ashura.S. Mnyachi - Mtendaji Kata Chihangu
32. Ndg.Asha F. Hasan - Mtendaji wa Kata Mikumbi
33. Ndg. Boke R. Mwita - Mtendaji wa Kata M/Mpelepele
34. Ndg. Ahmadi .R. Mtuli - Mtendaji wa Kata Mnyeu

35. Ndg. Lukia M. Abeid - Mtendaji wa Kata Chitekete
36. Ndg. Jamali .M. Mkaja - Mtendaji wa Kata Mtopwa
37. Ndg. Machacha Abdala - Mtendaji wa Kata Kitangari
38. Ndg. Salum A. Gheo - Mtendaji wa Kata Makukwe
39. Ndg. Omari A. Lyopoto - Mtendaji wa Kata Chiwonga
40. Ndg. Shaibu .H. Disusa - Mtendaji Kata Mkwedu
41. Ndg. Batuli B. Nahoda - Mtendaji wa Kata Mnyambe
42. Ndg. Faraji .K. Chiponda - Mtendaji wa Kata Nambali
43. Ndg. Mamlo A. Watu - Mtendaji wa Kata Mkoma II
44. Ndg. Meshack Litanda - K/ Afisa Mtendaji wa Kata Chilangala
45. Ndg. Abdul L. Masindano - Mtendaji wa Kata Maputi
46. Ndg.Selemani Aibu - Mtendaji wa Kata Mtunguru
47. Ndg. Jamila H. Nalinga - Mtendaji Kata Muungano
48. Ndg.Kanyoli A. Mnamala - Mtendaji wa Kata Mpwapwa.
49. Ndg Sharafi Mnandaje - Mtendaji wa Kata Nandwahi.

**WAGENI WAALIKWA.**

1. Ndg.Muhunzi Rashidi Katibu Chadema
2. Ndg. Omary .B. Ching'anganya Katibu CUF
3. Ndg. Lucy Ogutu Mtangazaji ITV - Mtwara
4. Ndg. Adamu Juma Mwandishi TBC Mtwara
5. Ndg. Haika Kimaro Mwandishi Gazeti la Mwananchi
6. Ndg. Cornel Antony Mwandishi Gazeti la Majira
7. Ndg. Juma Chikambu Mwandishi Newala FM Redio
8. SSP. Jonam Sande Mkuu wa Gereza Newala.
9. Ndg. Emmilya .A. Mwakyusa Afisa Uhamiaji Wilaya ya Newala

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Emmanuel Msuya - Afisa Utumishi
2. Ndg Rashidi Mabaya - Mwandishi wa Vikao.

**MUHTASARI NA 24 /2016/2017 : KUFUNGUA KIKAO:**

Mwenyekiti aliwasalimu na kuwakaribisha wajumbe, watendaji pamoja na wageni waalikwa katika mkutano wa baraza la madiwani robo ya nne 2016/2017 na kuwataka wajumbe kushiriki kikamilifu katika mkutano. Alifungua Mkutano saa 5:06 asubuhi.

**MUHTASARI NA 25/2016/2017: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Wajumbe walithibitisha agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe katika mkutano.

**MUHTASARI NA 26/2016/2017- KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 24/04/2017.**

Wajumbe walipitia muhtasari huo kwa umakini ukurasa hadi ukurasa na hakukuwa na marekebisho yaliyojitokeza na kuridhia muhtasari huo uwekwe saini ili uwe kumbukumbu sahihi ya mkutano wa baraza la madiwani.

**MUHTASARI NA 27/2016/2017- YATOKANAYO NA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 24/04/2017.**

Yatokanayo yalisomwa na kutolewa maelekezo ya utekelezaji kama ifuatavyo:-

Muhtasari Na. 14/2016/2017- Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo robo ya tatu 2016/2017.

*AZIMIO:*

Baraza la madiwani lipate mrejesho wa taarifa kuhusu nyumba ya mwalimu shule ya msingi muungano iliyotelekezwa.

*UTEKELEZAJI.*

Agizo limezingatiwa. Tume imebaini kuwa nyumba ya mwalimu shule ya msingi Muungano ilianza kujengwa baada ya kupokea fedha kutoka serikali kuu Tsh. 3, 100, 000/=. Kamati ya shule ilitangaza zabuni na mzabuni alipatikana na kutokana na kiasi cha fedha kilichotolewa na serikali kuu, mzabuni huyo alishindwa kukamilisha ujenzi. Lengo la kutoa kiasi hicho ni kuwa sehemu kubwa ya ukamilishaji ungechangiwa na wananchi jambo ambalo halikufanyika.

Wajumbe walipokea utekelezaji huo na kujadili kama ifuatavyo:-

Hoja ya Mhe. Menas Likuku, kutaka kufahamu nani aliyetelekeza nyumba ya mwalimu shule ya msingi muungano?

Ilijibiwa kuwa nyumba ya mwalimu shule ya msingi muungano imetelekezwa na jamii ya watu wa Muungano kwa kuwa wao ndio waliokuwa wanatakiwa kuchangia.

Hoja ya Mhe. Mohamedi Mnyolokoto kutaka kufahamu nyumba nyingine zilizojengwa na kukamilika pasipo kuchangiwa na wananchi inakuwaje hii ya muungano?

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema kuwa miradi hii inayotolewa fedha na serikali kuu haiwezi kujitosheleza hivyo inategemea ushirikiano kutoka kwa wananchi.

Mwenyekiti alisema Mkurugenzi pamoja na wataalamu wake waende kufanya tathmini ya jengo hilo la shule kuona kama litafaa au halitafaa kujengwa tena.

**MUHTASARI NA 28/2016/2017- MASWALI YA PAPO KWA PAPO.**

Mhe. Zaituni Nawanda alitaka kufahamu kipindi kilichopita asilimia 30% za Makusanyo zinazotakiwa kurudishwa kijijini walipokea 20% hivyo alitaka kufahamu 10% italipwa lini?
Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili Halmashauri yetu kwa sasa lakini litafanyiwa kazi.

Mhe.Mohamedi Mnyolokoto alisema kuwa wakati wa masika zahanati ya Mnali inavuja. Je? Halmashauri ya Wilaya inamkakati gani wa muda mrefu au muda mfupi wa kubadili bati zinazovuja?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa Halmashauri katika mipango yake imepanga kuboresha changamoto mbali mbali katika zahanati.

Mhe. Said Mawangwa alitaka kufahamu Halmashauri ya Wilaya kupitia idara ya afya ilifanya ukaguzi wa vyoo na matatizo mbalimbali yalibainika. Je? ni kiasi gani cha fedha kilipatikana kutokana na faini walizotozwa wananchi?

Mkurugenzi Mtendaji alisema taarifa itaandaliwa na Wah. Madiwani watapatiwa katika baraza la siku ya pili.

Mhe. Rashidi Lugomba alitaka kufahamu zahanati ya mpalu ina changamoto ya nishati ya umeme wa jua. je? Halmashauri inampango gani wa kuwapatia nishati hiyo ya jua.

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa kuwa katika bajeti hii kupitia vyanzo vya ndani vya mapato wataangalia uwezekano wa kuwapatia umeme wa jua.

Pia alimshauri Mhe. Diwani kuandaa harambee kupitia kwa wananchi, watendaji na waheshimiwa madiwani ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya maboresho ya zahanati ya Mpalu.

Swali la nyongeza kutoka kwa Mhe. Fabian Mahanyuka kuwa swali la Mhe. Rashidi Lugomba limezungumziwa zaidi ya mara mbili katika mkutano na halipati majibu inakuwaje?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa Halmashauri inachangamoto nyingi kutokana na uchache wa vyanzo vya mapato.

Mhe. Rashidi Nambomo alitaka kufahamu Halmashauri inampango gani wa kukamilisha ujenzi wa ofisi ya kata pamoja na samani za ofisi?

Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa zipo Changamoto nyingi zinazokabili ukamilishaji wa miradi kwa kuwa ruzuku kutoka serikali kuu hazipatikani kwa sasa. Alishauri ili kukamilisha miradi hii ni vema Waheshimiwa Madiwani wakashirikiana na wadau mbalimbali kuliko kusubiri serikali.

Swali la nyongeza kutoka kwa Mhe. Selemani Hiyari kuwa katika kabrasha kunaonekana bakaa zipo, kwa nini zisihamishiwe katika ujenzi wa ofisi hizo za kata?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa kulingana na sheria ya bajeti hairuhusiwi. Alimshauri Mhe. Diwani aanzishe jitihada za kuhamasisha ujenzi wa Kata kupitia nguvu za wananchi pamoja na wadau mbalimbali halafu Halmashauri itamuunga mkono.

Swali la nyongeza kutoka kwa Mhe. Jamali Nandonde kutaka kufahamu kuna jitihada gani za kupata watendaji wa vijiji baada ya watendaji waliokuwepo kuondolewa?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa lilishajadiliwa katika kikao cha Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na kupata idhini ya kikao cha Kamati ya fedha kuajiri vibarua kwa miezi mitatu na mchakato umeshaanza wa kuwapata watendaji wa vijiji na muda mfupi watapelekwa katika vijiji.

Mhe. Bakari Mniyopa alitaka kufahamu katika taarifa aliyosomewa Mkuu wa Mkoa wakati wa kuweka jiwe la msingi katika shule ya msingi malatu kuna ongezeko la fedha Tsh. milioni kumi na mbili. Je? Fedha hizo zilitoka wapi kwa kuwa wao kama Kata hawakuwa na taarifa.

Mkurugenzi Mtendaji alisema kiasi kilichoongezeka kilitoka Halmashauri kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo.

MUHTASARI NA 29/ 2016/ 2017- TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI.

Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya na kuijadili kama ifuatavyo:

*Uk1.*
Mhe. Rashidi Lugomba aliipongeza taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Newala kupata hati safi kulingana na ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali (CAG) za mwaka 2015/2016.

Pia alitaka kufahamu mabomba 73 yatagawanywa kwa utaratibu gani?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa serikali ilitoa maelekezo kuhusu ugawaji wa salfa tu.

Mjumbe alitaka kufahamu baada ya Watendaji kusimamishwa mishahara yao, je? kuna utaratibu gani wa kuwarudisha katika maeneo yao?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa wanasubiri maelekezo kutoka serikali kuu kuona nini cha kufanya.

Mhe. Diwani Mohamedi Mnyolokoto alitaka kufahamu katika kijiji husika akikosekana mwenye sifa ya kuomba utendaji wa kijiji itakuwaje?

Mkurugenzi Mtendaji alisema kijiji husika kinaweza kukosa mtu mwenye sifa lakini katika kata watapatikana wenye sifa kwa kuwa walioomba ni wengi.

*Uk 3:*
Mhe. Bakari Mniyopa alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji kwa kuwatengenezea barabara katika kata zao.

Pia alitaka kufahamu kipande cha barabara kilichoharibiwa na TANROAD katika Kata ya Malatu na Mkurugenzi Mtendaji alisema atawaandikia barua, je? Utaratibu wa kuwaandikia barua umefikia wapi?

Mkurugenzi Mtendaji alijibu kuwa barua ilishawaandikia kwa ajili ya kuwakumbushia.

Hoja ya Mhe. Rashidi Songoni kutaka kufahamu watumishi wa Idara tatu, Mhandisi, Mipango na Manunuzi, pamoja na Fedha na Utawala wanatoka wapi? na ofisi itakuwa wapi?

Ilijibiwa na Mkurugenzi Mtendaji kuwa wataalamu hao wataazimwa kutoka Halmshauri ya Wilaya kwa muda na ofisi yao itakuwa pale ilipo Idara ya Ujenzi kwa sasa.

Hoja ya Mhe. Hanafi Nahonyo kutaka kufahamu je? Watumishi wa TARURA watawajibika kwa nani?

Ilijibiwa na Mkurugenzi Mtendaji kuwa ni wakala anayejitegemea.

Hoja ya Mhe.Jamali .J. Nandonde kutaka kufahamu katika harambee ya kuchangia Mnyambe sekondari kiasi gani cha fedha kilichopatikana?

Ilijibiwa na Mkurugenzi Mtendaji kuwa taarifa itaandaliwa na Wah. Madiwani. watapatiwa siku ya baraza la pili

Hoja ya Mhe. Selemani Mtili kutaka kufahamu kuna taarifa zilizosambaa kuwa Mnyambe kuna choo kimejengwa kwa shilingi milioni themanini (80) je? hii taarifa ikoje?

Mkurugenzi Mtendaji alisema taarifa hizo sio za kweli choo kile hakina thamani ya milioni themanini japo ni choo cha kisasa kilichojengwa hata wataalamu kutoka Mkoani walikisifia pamoja na kukipongeza, alishauri Wah. Madiwani kwenda kutembelea na kuona nini kinachofanyika Mnyambe sekondari.

Pia Wah. Madiwani wasiwe watu wa kufifisha jitihada zinazofanywa na watendaji na kuwataka kuwa mabalozi wazuri wa kuwaelimisha wananchi.

**MUHTASARI NA 30/2016/2017- TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA.**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala aliwasilisha taarifa yake, wajumbe waliipokea na kuijadili kama ifuatavyo:-

Hoja ya Mhe. Selemani Mtili alitaka kufahamu katika kikao hicho suala la mizani lilijadiliwa vipi?

Ilijibiwa kuwa ni kweli suala la mizani lilijadiliwa na kusisitizwa kuwa kabla ya kupeleka korosho kwenye mizani wahakikishe wanazikausha ndipo wapeleke kwenye mizani.

Pia watahakikisha kuwa patakuwepo na wataalamu wa kuzikagua na kuzirekebisha pale zinapoharibika.

Mhe. Hanafi Nahonyo alimwomba Mwenyekiti awaambie Idara ya Kilimo kuhakikisha inawaelimisha wananchi kufungua akaunti mapema

Mwenyekiti alisema ni jukumu la Wah. Madiwani kuwaelimisha wananchi juu ya kufungua akaunti.

**MUHTASARI NA 31/2016/2017 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA NNE 2016/2017.**

Afisa Mipango Wilaya aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya nne kwa kusema kuwa katika mwaka 2016/2017 Halmashauri inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya shilingi 11,899,130,924/= kati ya hizo shilingi 934,707,803/= ni fedha za bakaa ya mwaka 2015/2016, na shilingi 10,964,423,121 ni fedha idhinishwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ikiwa inajumuisha mapato ya ndani, ruzuku kutoka serikali kuu na fedha kutoka kwa wahisani.

Hadi kufika tarehe 30 juni, 2017 Halmashauri imepokea jumla ya shilingi 6,671,196,438. Fedha zilizopokelewa kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo ni sawa na asilimia 61 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, Halmashauri imepokea Tshs. 259,000,000/= kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya Sekondari ya Mnyambe.

Hadi Juni 30, 2017, Halmashauri imeshatumia jumla ya shilingi 7,478,703, 209/= katika kutekeleza miradi katika sekta mbalimbali. Matumizi haya yamehusisha fedha za bakaa na fedha zilizopokelewa kwa bajeti ya mwaka husika.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kama ifuatavyo:

*UK 3:*
Hoja ya Mjumbe kutaka kufahamu kuwa kwa nini bakaa inakuwa nyingi wakati kuna miradi mingine haijatekelezwa?

Ilijibiwa kuwa miradi yetu inafadhiliwa na kerikali Kuu na wakati mwingine fedha hizi zinapokelewa mwishoni mwa mwaka hivyo kufanya fedha hizo zibaki kwa mwaka husika na utekelezaji wake kuingia mwaka mwingine wa fedha.

Hivyo fedha hizo za bakaa hutumika katika utekelezaji wa miradi husika na si vinginevyo kwa sababu fedha hizo zinakuja kwa maelekezo.

**Uk 10:**
Hoja wa mjumbe kutaka kufahamu kwa nini fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwezesha ujenzi ya wodi ya wagonjwa katika kituo cha Afya Chihangu Tsh. 14,000,000/= hazikutolewa wakati wananchi wa Chihangu wanashida ya huduma ya Afya?

Ilijibiwa kuwa fedha zilizopokelewa 2016/2017 za CDG zilisisitizwa kuwa zipelekwe kukamilisha miradi viporo na si vinginevyo na kwa kuwa mradi wa Chihangu ni mpya ndio sababu iliyopelekea mradi huo kutopelekewa fedha.

Hoja ya Mjumbe kutaka kufahamu kituo cha Afya Mkwedu mwanzoni kilipangiwa Tsh, 25,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba moja ya Mtumushi ikapunguzwa hadi kufikia Tsh.14, 000,000/= na bado fedha hizo hazijatolewa, hii inasababishwa na nini?

Ilijibiwa kuwa Serikali Kuu haikuleta fedha hizo na fedha kidogo zilizopokelewa zimepelekwa kwenye miradi viporo kama ilivyoelekezwa na miradi ambayo haijatekelezwa imewekwa kwenye bajeti 2017/2018 hivyo fedha zikiletwa itatekelezwa.

*Uk 16:*
Ujenzi wa Zahanati Mnyambe imepelekwa Tsh.200,000/= Je fedha hizo mbona ni kidogo? zitafanya kitu gani?

Ilijibiwa kuwa ni vema akashukuru kwa kidogo kilichopatikana. Fedha hizo ni kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mradi pale ambapo wananchi wameanza utekelezaji. Hivyo mradi huo umepata mifuko 80 ya saruji pamoja na Fedha Tsh.200, 000/=

Mhe. Mbunge alishauri fedha / vifaa zinazotokana na mfuko wa jimbo zikipelekwa katika vijiji vilivyopitishwa, wananchi waambiwe kabisa huo ni mchango wa mbunge ili waweze kufahamu mchango wa mbunge katika shughuli za kimaendeleo.

*Uk 17:*
Mjumbe alitaka kufahamu kwa nini Mradi wa Mnauya - Mmulunga maji hayapatikani kama inavyotakiwa?

Ilijibiwa kuwa ni kweli Mradi huo umekamilika na ili maji yapatikane kwa uhakika ni lazima miundombinu iwe vizuri na salama. Pia Mamlaka ya Maji Makonde hutoa maji kwa ratiba na sio kila siku.

Mjumbe alitaka kufahamu nini mipango ya muda mfupi ili maji yaweze kupatikana.

Ilijibiwa mipango ya muda mfupi ni kuendelea kuikarabati laini hiyo ya maji na kama Mhandisi Mkazi wa Mamlaka ya Maji Makonde atakuwa na mabomba hayo watashirikiana katika kufanya kazi ya kuyaweka katika eneo husika.

*Uk 18:*

Mjumbe alitaka kufahamu ni lini mradi wa maji makukwe utakamilika ili wananchi wapate maji?

Ilijibiwa kuwa mradi wa Maji Makukwe kwa sehemu kubwa umekamilika kilichobaki ni kuweka mabomba ya Km. 1.4 na mabomba hayo yameshaagizwa.

Pia Mkandarasi anatakiwa kulipwa kwa sehemu aliyokamilisha lakini mpaka sasa Serikali haijaleta fedha hizo.

Hoja ya mjumbe kutaka kufahamu Halmashauri ina mpango gani wa kukarabati mabomba chakavu Mnyambe - Chihangu?

Ilijibiwa kuwa mamlaka ya ukarabati wa mabomba hayo ni ya Halmashauri lakini fedha iliyotarajiwa kukarabati mabomba hayo ilipelekwa kwa mamlaka ya maji makonde na haipo chini ya Halmashauri.

Mhe. Mbunge alishauri kuwa Mhandisi wa Halmashauri kushirikiana na Mhandisi Mkazi katika kuweka mipango ya dharura..

Mhandisi alijibu kuwa suala hilo linahitaji rasilimali fedha na kwa sasa rasilimali fedha hakuna, kuhusu ushirikiano na Mhandisi Mkazi ushauri huo umezingatiwa.

Hoja ya Mjumbe kutaka kufahamu matengenezo ya kawaida barabara za Mkoma I - Mnyambe - Miyuyu, barabara hizo zimewekwa vifusi na kufanya barabara isipitike je? ni lini itakamilika?

Mhandisi alijibu Mradi huo ulitarajiwa kukamilika tarehe 30/08/2017 na kwa sasa barabara hizo zipo upande wa TARURA.

Mjumbe alitaka kufahamu barabara ambazo utengenezaji wake unategemea mfuko wa jimbo ni lini zitashughulikiwa?

Ilijibiwa kuwa utaratibu wa manunuzu na kumtafuta mzabuni unaendelea kufanyika na mfumo ukifunguliwa barabara hizo zitafanyiwa kazi.

**MUHTASARI NA 32/2016/2017- KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KATA ROBO YA NNE 2016/2017.**

Taarifa zilikusanywa na kuwasilishwa kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

**MUHTASARI NA 33/2016/2017- KUPITIA NA KUPITISHA RATIBA YA VIKAO VYA HALMASHAURI KWA MWAKA MPYA WA FEDHA 2017/2018.**

Afisa Utumishi na Utawala aliwasilisha ratiba ya vikao vya Halmashauri ya Wilaya ya Newala kwa mwaka mpya wa fedha 2017/2018.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kushauri kuwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ijitahidi ratiba ifuatwe.

Ilielezwa kuwa wakati mwingine ratiba haifuatwi kutokana na kuwa shughuli nyingi zinaingiliana na kufanya ratiba kubadilishwa badilishwa.

**MUHTASARI NA 34/2016/2017-KUFUNGA MKUTANO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
Alishukuru Mungu kwa kumaliza Mkutano vizuri. Alisema kuwa michango ya Wah. Madiwani imepokelewa na itafanyiwa kazi, hivyo wamuombe mungu serikali ilete fedha kwa wakati ili waweze kukamilisha mradi yao.

Pia aliwashukuru Wah. Madiwani kwa ushirikiano wao kwa kipindi chote cha mwaka mzima na kuwaomba uendelee hivyo hivyo kwa mwaka mpya wa fedha unaoanza.

**MWENYEKITI WA HALMASHAURI (W)**
Alimshukuru mungu kuwawezesha kumaliza Mkutano. Pia alisisitiaza mambo yafuatayo:-

**Ukamilishaji wa miradi viporo :** aliwaomba Wah. Madiwani kujitahidi kuleta taarifa sahihi za miradi ili itengewe bajeti yenye uhalisia kwa ajili ya kumalizia miradi hiyo.

**Mahusiano**: ili kuendeleza mahusiano mazuri taarifa za utekelezaji wa miradi yao wanazozipata nje ya ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ni vyema kufika ofisi ya Mkurugenzi au Mwenyekiti na kupata majibu yaliyosahihi. Alifunga mkutano saa 8:57 mchana.

"UMETHIBITISHWA"

MWENYEKITI: KATIBU:

JINA: CHIWANGA R. NDEMBO JINA: MUSSA N. CHIMAE

SAINI:........................... SAINI:...........................

TAREHE: 01. 11. 2017

**Mahusiano**: ili kuendeleza mahusiano mazuri taarifa za utekelezaji wa miradi yao wanazozipata nje ya ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ni vyema kufika ofisi ya Mkurugenzi au Mwenyekiti na kupata majibu yaliyosahihi. Alifunga mkutano saa 8:57 mchana.

"UMETHIBITISHWA"

| | |
|---|---|
| MWENYEKITI: | KATIBU: |
| JINA: CHIWANGA R. NDEMBO | JINA: MUSSA N. CHIMAE |
| SAINI: [signature] | SAINI: [signature] |

TAREHE: 01. 11. 2017

**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA NNE 2016/2017 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA NEWALA TAREHE 31/07/2017.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Chitwanga R. Ndembo | - Diwani Mtunguru | -Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. | Musa M. Chimae | - Mkurugenzi Mtendaji | -Katibu |
| 3. | Mhe. | Rashid A. Akbar | - Mbunge Newala (V) | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. | Swalehe F. Amri | - Diwani Chitekete | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. | Salehe M. Kamtwanje | - Diwani Mpwapwa | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. | Hashimu B. Namawa | - Diwani M/Mpelepele | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. | Mohamed A. Mnyolokoto | - Diwani Muungano | -Mjumbe |
| 8. | Mhe. | Shaibu R. Ngumbe | - Diwani Kitangari | -Mjumbe |
| 9. | Mhe. | Zaituni L. Nawanda | -Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 10. | Mhe. | Saidi Y. Mawangwa | - Diwani Makukwe | -Mjumbe |
| 11. | Mhe. | Menas M. Likuku | - Diwani Maputi | -Mjumbe |
| 12. | Mhe. | Bakari C. Mniyopa | - Diwani Malatu | -Mjumbe |
| 13. | Mhe. | Amina Mkanangwamba | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 14. | Mhe. | Sauda R. Rashidi | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 15. | Mhe. | Athumani M. Mniwasa | -Diwani Chiwonga | -Mjumbe |
| 16. | Mhe. | Munga Mohamedi | - Diwani Mchemo | -Mjumbe |
| 17. | Mhe. | Jamali J. Nandonde | - Diwani Chilangala | -Mjumbe |
| 18. | Mhe. | Rashidi B. Songoni | - Diwani Chihangu | -Mjumbe |
| 19. | Mhe. | Fabian J. Mahanyuka | - Diwani Mnyambe | -Mjumbe |
| 20. | Mhe. | Hanafi N. Nahonyo | - Diwani Mtopwa | -Mjumbe |
| 21. | Mhe. | Rashidi H. Lugomba | - Diwani Nakahako | -Mjumbe |
| 22. | Mhe. | Raia R. Nang'oko | - Diwani Mikumbi | -Mjumbe |
| 23. | Mhe. | Yahaya A. Lisinge | - Diwani Nandwahi | -Mjumbe |
| 24. | Mhe. | Rashidi Nambomo | - Diwani Mnyeu | -Mjumbe |
| 25. | Mhe. | Selemani M. Hiyari | - Diwani Mkoma II | -Mjumbe |
| 26. | Mhe. | Maua Makubui | -Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 27. | Mhe. | Zainabu R. Mpita | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 28. | Mhe. | Zakina A. Mduma | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 29. | Mhe. | Arabia H. Mkwatile | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 30. | Mhe. | Simon F. Nachingulu | - Diwani Nambali | -Mjumbe |
| 31. | Mhe. | Hadija M. Likwembe | - Diwani/V/Maalum | -Mjumbe |
| 32. | Mhe. | Selemani A. Mtili | - Diwani Mkwedu | -Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA** - Hakuna

**WATAALAMU WALIYOHUDHURIA.**

1. Ndg. Shakira Ahmadi –Afisa Utumishi (W)
2. Ndg. Sylvester A. Balama - Mhandisi Ujenzi (W)

3. Ndg. Innocent Magayane - K/Mweka Hazina (W)
4. Ndg. Benaya Sanane - Mchumi
5. Ndg. Christina Kambuga - Afisa M/Jamii (W)
6. Ndg. Ndg. Msafiri Ngai - Afisa Ugavi
7. Ndg. Wilson F. Mafumba - Mkaguzi wa Ndani (W)
8. Ndg. Magreth Likonda - Afisa Ardhi,Maliasili na Mazingira (W)
9. Ndg. Kalugendo Majidu - Afisa Elimu Sekondari (W)
10. Ndg.Nsajigwa Sadiki - kaimu Mhandisi wa Maji (W)
11. Ndg. Nsajigwa Mkwatika - Kaimu Katibu TSC (W)
12. Ndg. Mahundu Innocent - Afisa Ushirika (W)
13. Ndg. Omary Msuya - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
14. Ndg. Rogers Muganyizi - Afisa Ardhi (W)
15. Dr. Judith Ringia - Mganga Mkuu (W)
16. Ndg. Benjamini Macha - Kaimu Mratibu CHF (W).
17. Ndg.Yusufu S.Mshamu - Afisa Tarafa Chilangala.
18. Ndg.Jamila Nalinga - Mtendaji Kata Muungano.
19. Ndg.Boke Mwita - Mtendaji Kata M/Mpelepele.
20. Ndg.Frank Ntilla - K/Mratibu wa UKIMWI
21. Ndg.Shada Nankoko - K/Afisa Utamaduni
22. Ndg.Samuli A. Ali - K/Mtendaji Kata Mkwedu
23. Ndg.Mussa Mohamedi - K/Mtendaji Kata Mpwapwa
24. Ndg.Selemani Aibu - Mtendaji Kata Mtunguru
25. Ndg.Musa E. Musoma - K/Afisa Elimu Sekondari
26. Ndg.Batuli Nahoda - Mtendaji Kata Mnyambe
27. Ndg.Victoria Lusana - Afisa Tarafa Kitangari
28. Ndg.Agness Mnipalika - Mtendaji Kata Mchemo
29. Ndg.Rukia M. Abeid - Mtendaji Kata Chitekete
30. Ndg.Omari Lyopoto - Mtendaji Kata Chiwonga
31. Ndg.Saidi Ussi - Mtendaji Kata Mnyeu
32. Ndg.Hamisi J. Saidi - K/Mtendaji Kata Mikumbi
33. Ndg. Alford Mpanda - Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W)
34. Ndg.Faraji K. Chiponda - Mtendaji Kata Nambali
35. Ndg.Haulii H. Hamisi - Mtendaji Kata Malatu
36. Ndg.Salumu Hassani - Mtendaji Kata Mtopwa
37. Ndg.Amina Mbelenje - K/Mtendaji Kata Maputi
38. Ndg.Selemani Chivambo -K/Mtendaji Kata Nakahako
39. Ndg. Machacha Abdala - Mtendaji Kata Kitangari
40. Ndg. Halfani Halfani - Mtendaji Kata Nandwahi
41. Ndg.Salumu Gheo - Mtendaji Kata Makukwe.
42. Ndg.Emmanuel Msuya - Afisa Utumishi.

**WAGENI WAALIKWA**

1. Ndg. Nuru Ringo - Afisa Serikali za Mitaa Mkoa
2. Ndg. Paulo Simwela - K/Katibu Tawala.
3. Ndg. Joseph Molel - NMB

4. Ndg. Ally A. Lilama - Mwenyekiti CCM (W)
5. Ndg. Sofia Kibaba - K/Katibu CCM (W)
6. Ndg. Shabani N. Fungameza -K/Afisa Uhamiaji (W)
7. Ndg. Edwin R. Kazingo - Meneja Maji Makonde
8. Ndg. Clemence Kifutumo - Fundi Mamlaka Makonde
9. Ndg. Kanunga Shabani - Katibu CUF (W)
10. Ndg. Edward L. Mukama - Kamanda TAKUKURU (W)
11. Ndg. Dennis Masanja - Afisa Usalama (W)
12. Ndg. Jonam Sande - Mkuu +wa Gereza (W)
13. Ndg. Mange Sagudah - Meneja NMB
14. Ndg. Edward P.M Msilikali - Mkuu wa Polisi (W)
15. Ndg. Lucy Ogutu - Mwandishi wa Habari ITV
16. Ndg. Marry Sanyiwa - Mwandishi wa Habari
17. Ndg. Adam Juma - Mwandishi wa Habari TBC
18. Ndg. Mohamed Mwaya - Azam Media LTD
19. Ndg. Cornel Anthony - Majira Mtwara.

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Rashid Mabaya - Mwandishi wa vikao.

**MUHTASARI NA.13/2016/2017: KUFUNGUA MKUTANO:**

Mwenyekiti aliwasalimu Wajumbe na wageni waalikwa na kuwakaribisha katika Mkutano wa Baraza la Madiwani. Alifungua Mkutano saa 5:25 asubuhi.

**MUHTASARI NA.14/2016/2017: KUTHIBITISHA AGENDA:**

Wajumbe walithibitisha agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe katika kikao.

**MUHTASARI NA.15/2016/2017: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 24/04/2017:**

Wajumbe walipitia Muhtasari kwa umakini ukurasa hadi ukurasa na hakukuwa na marekebisho yaliyofanyika.

Wajumbe waliupokea muhtasari na kuridhia uwekwe saini ili uwe kumbukumbu sahihi ya kikao.

**MUHTASARI NA 16/ 2016/2017: TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU.**

**KAMATI YA MAADILI.**

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na hakukuwa na majadiliano.

fedha zinazoletwa na uhalisia wa mifugo inayochinjwa katika vijiji na Kata haulingani.

Katika kikao hicho kamati ilipitisha majina 31 ya watumishi waliopendekezwa kwenda masomoni kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo watendaji wa vijiji hawakuruhusiwa kwenda masomoni kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 hadi pale watendaji wa vijiji watakapoajiriwa kutokana na vijiji vingi kutokuwa na watendaji.

**KIKAO CHA TAREHE 14/09/2017.**

Wajumbe walipokea taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mwezi Agosti ambapo fedha jumla ya Tshs 2,704,228,571.19 zilipokelewa. Aidha Matumizi kwa Mwezi Julai yalikuwa ni jumla ya Tshs 2,084,636,320.18 .Kamati ilipokea taarifa hiyo na kushauri kuwa:

Katika kuboresha mapato yanayotokana na mifugo menejimenti ifanye vikao na watendaji wa vijiji na wafanyabiashara wanaouza nyama ili kuhakikisha ushuru unaotokana na nyama unapatikana wa kutosha na kuongeza pato la Halmashauri.

Kamati pia ilisisitiza kuhusu usimamizi wa mazao mchanganyiko kwa kuwa bado kuna mapungufu ambapo wafanyabiashara wengi hawalipi ushuru.

Kabla ya kupitisha taarifa ya Mpango wa manunuzi kwa mwaka 2017/2018 kamati iliagiza kuwa taarifa hiyo ichanganuliwe kwa kila idara na kwa kila robo ili kuweza kufahamu kuwa kila idara inatumia kiasi gani na vifaa kiasi gani kwa kila robo mwaka.

Pia kamati ilipokea taarifa ya Halmashauri kuingia Mkataba wa ulinzi na Mshauri wa majeshi ya akiba kwa ajili ya kulinda mali za Halmashauri na kushauri kwamba Halmashauri ni bora iinhie mkataba na mgambo wenyewe kuliko kuingia mkataba na mshauri wa majeshi ya akiba kwa kuwa yeye hajasajiliwa kwa kutoa huduma ya ulinzi.

**KIKAO CHA TAREHE 28/10/2017.**

Wajumbe walipokea taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mwezi Septemba 2017 ambapo fedha jumla ya Tshs 2, 55,777,809.28 zilikusanywa toka vyanzo mbalimbali .Aidha Matumizi kwa Mwezi Septemba 2017 yalikuwa ni jumla ya Tsh 2,875,148,446.71 kama ilivyochanganuliwa kwenye jedwali.

*Jedwali 1: Mapato:*

| AINA YA MAPATO | MAPATO MWEZI SEPTEMBA 2017 |
|---|---|
| Albaki ya mwezi **AGOSTI 2017** | 1,412,294,937.21 |
| **MAPATO YA SEPTEMBA 2017** | |
| Mapato ya Kata Jedwali Na.2 | 13,312,982.00 |
| Ruzuku Matumizi ya Kawaida-Utawala | - |
| Mapato ya Ofisi Kuu (Own Source) | 16,221,781.30 |
| Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida na mitihani | - |
| Ruzuku ya Mishahara | 1,348,535,000.00 |
| Mifuko mbalimbali jedwali na 3 | 877,708,045.98 |
| **JUMLA** | **2,255,777,809.28** |
| **JUMLA KUU YA MAPATO** | **3,668,072,746.49** |

*Jedwali 2: Matumizi:*

| S/N | MAELEZO | MATUMIZI SEPTEMBA 2017 |
|---|---|---|
| 2.1 | Maeneo yanayopata Ruzuku | |
| | (1) Mishahara | 1,329,814,785.74 |
| | (2) Matumizi ya Kawaida | 119,368,750.00 |
| | JUMLA YA MATUMIZI YA RUZUKU | |
| **2.2** | **Maeneo yasiyo na Ruzuku** | |
| | (1) Mishahara (PE) | |
| | (2) Matumizi ya Kawaida | 29,312,882.00 |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YASIYO YA RUZUKU** | |
| | (3) Matumizi Mifuko mbalimbali | 1,396,652,028.97 |
| | **JUMLA KUU YA MATUMIZI** | **2,875,148,446.71** |
| | **SALIO LA SEPTEMBA 2017** | **792,924,299.78** |

Kamati ilipokea taarifa hiyo na kushauri yafuatayo:

- Wajumbe walishauri kuwa watumishi kutoka ofisi kuu wanapokuwa katika ziara ya kikazi vijijini wahakikishe wanafanya ukaguzi kwa baadhi ya vyanzo vya mapato kama vile uchinjaji kuhakikisha ushuru unalipwa.
- Mweka Hazina ahakikishe watumishi wanaolipwa mishahara kupitia vyanzo vya mapato vya ndani wanalipwa.
- Ili kuhakikisha kuwa ushuru haupotei Mweka Hazina afuatilie ukusanyaji ulivyofanyika kwenye kijiji cha Idamnole kata ya Chihangu na taarifa iwasilishwe kikao kijacho.

Kamati pia ilipitia taarifa ya Mkaguzi wa ndani robo ya kwanza 2017/2018 na kuagiza kuwa kila mwenye hoja yake ahakikishe kuwa anatafuta viambata vyake ili hoja zifutwe.

Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na taarifa ya kutembelea miradi mbalimbali ya ujenzi kama ifuatavyo:

- Mradi wa maji Mitema-Machenje (Utandazaji wa mabomba mapya) kamati iliagiza wataalamu wa maji wa Halmashauri kuhakikisha wanamsimamia mkandarasi aweze kukamilisha mradi mapema.

- Mradi wa soko la kijiji cha Makukwe kamati ilishauri kuwa fedha za umaliziaji wa soko zisipelekwe mpaka pale utakapotolewa mchanganuo wa matumizi ya fedha za awali zilizopelekwa katika mradi huo.

- Mradi wa shule ya Msingi Muungano kijiji cha Mmovo kamati ilishauri kuwa ujenzi wa darasa hilo ukamilike ndani ya mwezi mmoja ili darasa liweze kutumika

- Kamati pia ilitembelea mradi wa shule ya msingi Matale(Chiuta) ambapo ilishauri kuwa ujenzi wa darasa hilo ukamilike ndani ya mwezi mmoja ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo.

Pia wajumbe walipokea taarifa ya kuanzishwa kwa duka la dawa na vifaa tiba litakalo hudumia vituo vya afya katika Halmashauri na kueleza kuwa lengo la kuanzishwa kwa duka hili ni zuri sana lakini walishauri mkakati uanzishwe wa duka hilo kulihamishia Newala vijijini ( kitangari,Mkwedu au Chihangu) ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mwisho kamati ilipokea taarifa ya watumishi wa ajira mpya waliopitishwa na bodi ya ajira ya Halmashauri ya Wilaya ya newala kwa kada za Watendaji wa Vijiji,Madereva pamoja na makatibu mahsusi na majina yaliyochaguliwa yalipitishwa.

Naomba Kuwasilisha

CHITWANGA R.NDEMBO
MWENYEKITI
KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO.
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA.

**KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Mwenyekiti wa Kamati ya kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa ya kamati yake. Mjumbe alihoji kwa nini kwenye taarifa ya Kamati ya Ukimwi haionyeshi taarifa ya Taasisi zingine tofauti na NEWNGONET?

Mwenyekiti alijibu kuwa robo tatu zilizopita taarifa zilikuwa zinawasilishwa za taasisi zote lakini ni robo hii ya nne ndiyo imewasilishwa taarifa moja ya NEWNGONET.

**KAMATI YA ELIMU,AFYA NA MAJI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu,Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya kamati yake.

Wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alihoji kuwa hadi sasa kupitia kamati ya Elimu,Afya na Maji ni madarasa mangapi na nyumba ngapi hazijakamilika?

Afisa Elimu alijibu kuwa hadi sasa kuna miradi vipolo inakamilishwa hivyo miradi hiyo ikikamilika taarifa ya miradi isiyokamilika itatolewa.

Mjumbe alihoji ni maeneo gani korofi yamerekebishwa ili wananchi waweze kupata huduma ya Maji?

Mhandisi alijibu kuwa sehemu korofi zilizorekebishwa ni Mitema - Nanda na Mnuwi - Chiwambo.

Mjumbe alihoji je hadi sasa baada ya ukarabati wa eneo la Malatu - Mdimba maji yanatoka?

Mwenyekiti wa Kamati alijibu kuwa tatizo ni jenereta ndilo linalosababisha wananchi wasipate maji kwa sasa.

Mjumbe alihoji kutaka kufahamu je kiasi cha fedha kilichopelekwa Mamlaka ya Maji Makonde kupitia Halmashauri kimefanya kazi gani hadi sasa?

Meneja wa Mamlaka ya Maji Makonde alijibu kuwa kiasi cha fedha kilichopokelewa ni shilingi bilioni 2.
Kiasi tajwa kimeletwa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa sehemu korofi ambapo kipande cha Chihangu - Mnyambe ni km 8 kwa bomba la inchi 3
Kununua pampu 2 Mitema.

Mjumbe alihoji je Kama pampu itafungwa Mitema na kupeleka Maji Mtongwele,maji hayo yatapelekwa kwa njia gani wakati mabomba ni mabovu?
Meneja wa Makonde alijibu kuwa kwa sasa maeneo ya Mradi yote ni chakavu,hivyo kwa hali hiyo jinsi ilivyo italazimika kufanya ukarabati wa sehemu korofi tu.

Mjumbe alihoji hadi sasa bilioni 2 ya ukarabati wa miundombinu ya maji imefikia wapi?

Meneja wa Maji Makonde alijibu kuwa hadi sasa Mikataba imeshasainiwa na kinachosubiliwa ni Mkandarasi kuleta vifaa na kuanza kazi.

Meneja alisema kuwa sehemu zote korofi zimebainishwa na zitafaniwa kazi.

**KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya kamati yake.

Wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alihoji je Halmashauri ina mpango gani wakuwaunga mkono wananchi wa Mitema waliyojitolea kurekebisha daraja la kipande cha Mtongwele - Mitema?

Mhandisi wa Ujenzi alijibu kuwa Halmashauri imetenga kiasi cha pesa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuweka makalavati katika eneo la Mitema - Mtongwele.

Mjumbe alihoji kwa nini kwenye kata zingine barabara zimechongwa zote na kata zingine barabara hazijachongwa?

Mhandisi wa Ujenzi alijibu kuwa changamoto ya fedha ndiyo inayosababisha baadhi ya maeneo kuchelewa kuchongwa barabara hizo.

Mjumbe alisema kuwa taarifa zilizopo ni kuwa kila mkulima wa korosho anatakiwa kufungua akauti benki ili malipo yapitie benki, je taratibu zipoje?

Meneja wa NMB alijibu kuwa kwa agizo la Mkuu wa Mkoa linamtaka kila mkulima afungue akaunti benki. Uhamasishaji umefanyika na wananchi wameelewa.

Changamoto kubwa ni kuwa wakulima wengi wanasema uzalishaji wao ni mdogo hivyo hawataweza kufungua akaunti.

Aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kufungua akaunti.

Meneja wa NMB alisisitiza kuwa kwa wale wakulima waliyo mbali na benki ya NMB kwa sasa mawakala wa NMB wapo kila sehemu hivyo huduma za kibenki zitapatikana kupitia mawakala waliyopo vijijini.

Mjumbe alihoji je kuna mpango gani wa kuanzisha eneo la Chilolelo lililopo Chilangala kuwa katika maeneo ya Utalii?

Mkuu wa Idara ya Maliasili alijibu kuwa hatua zikifuatwa inawezekana kwani kwenye zoezi la kukamilisha linahitaji fedha kwa ajili ya Kuliendeleza eneo kwa miundombinu.

Meneja wa Maji Makonde alijibu kuwa hadi sasa Mikataba imeshasainiwa na kinachosubiliwa ni Mkandarasi kuleta vifaa na kuanza kazi.

Meneja alisema kuwa sehemu zote korofi zimebainishwa na zitafaniwa kazi.

**KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya kamati yake.

Wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo:

Mjumbe alihoji je Halmashauri ina mpango gani wakuwaunga mkono wananchi wa Mitema waliyojitolea kurekebisha daraja la kipande cha Mtongwele - Mitema?

Mhandisi wa Ujenzi alijibu kuwa Halmashauri imetenga kiasi cha pesa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuweka makalavati katika eneo la Mitema - Mtongwele.

Mjumbe alihoji kwa nini kwenye kata zingine barabara zimechongwa zote na kata zingine barabara hazijachongwa?

Mhandisi wa Ujenzi alijibu kuwa changamoto ya fedha ndiyo inayosababisha baadhi ya maeneo kuchelewa kuchongwa barabara hizo.

Mjumbe alisema kuwa taarifa zilizopo ni kuwa kila mkulima wa korosho anatakiwa kufungua akauti benki ili malipo yapitie benki, je taratibu zipoje?

Meneja wa NMB alijibu kuwa kwa agizo la Mkuu wa Mkoa linamtaka kila mkulima afungue akaunti benki. Uhamasishaji umefanyika na wananchi wameelewa.

Changamoto kubwa ni kuwa wakulima wengi wanasema uzalishaji wao ni mdogo hivyo hawataweza kufungua akaunti.

Aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kufungua akaunti.

Meneja wa NMB alisisitiza kuwa kwa wale wakulima waliyo mbali na benki ya NMB kwa sasa mawakala wa NMB wapo kila sehemu hivyo huduma za kibenki zitapatikana kupitia mawakala waliyopo vijijini.

Mjumbe alihoji je kuna mpango gani wa kuanzisha eneo la Chilolelo lililopo Chilangala kuwa katika maeneo ya Utalii?

Mkuu wa Idara ya Maliasili alijibu kuwa hatua zikifuatwa inawezekana kwani kwenye zoezi la kukamilisha linahitaji fedha kwa ajili ya Kuliendeleza eneo kwa miundombinu.

**KAMATI YA FEDHA,UTAWALA NA MIPANGO**

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

**Uk 3**
Mjumbe alihoji kwa nini kwenye taarifa ya mapato haionyeshi mapato ya Redio?.

Mwenyekiti wa kamati alijibu kuwa mapato ya redio yapo kwenye mapato ya ofisi kuu.

Mjumbe alihoji kuwa taarifa inaonyesha makusanyo ya Halmashauri ni asilimia 81% kwa nini hali ya kifedha siyo nzuri?

Mwenyekiti wa kamati alijibu kuwa hali ya kifedha ni kweli siyo nzuri kwani kwa sasa Halmashauri hujiendesha kwa mapato ya ndani, Ruzuku haijaletwa, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kusimamamia na kuhamasisha ulipaji wa ushuru wa Halmashauri.

Mjumbe alihoji kwa nini Kata ya Mpwapwa na Kitangari zipo chini kimakusanyo?

Mwenyekiti wa Kamati alijibu kuwa Kata hizo zilikadiliwa fedha kubwa kuliko maeneo au ukubwa kata.

---

**MUHTASARI NA 17/2016/2017: UCHAGUZI WA MAKAMU MWENYEKITI NA UUNDAJI WA KAMATI MBALIMBALI.**

Mkurugenzi Mtendaji aliendesha uchaguzi huo:
Alisema kuwa amepokea barua toka kwa Katibu wa CCM iliyoleta jina la Makamu mwenyekiti ambaye ni ndg. SWALEHE F. AMRI na Chama cha CUF ni ndg. SAUDA R. RAJABU.

Mjumbe alihoji je kanuni inaruhusu Mheshimiwa Diwani Viti maalumu kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti?

Afisa Sheria alijibu kuwa kanuni inaruhusu, kanuni inasema mgombea anatoka miongoni mwa Waheshimiwa Madiwani.

Msimamizi wa Uchaguzi aliwataka wajumbe wenyeviti wa Kamati wajiuzulu nyazifa zao.
Uchaguzi uliendelea na msimamizi alitoa matokeo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa ZAUDA R. RAJABU amepata kura 3
Mheshimiwa SWALEHE F. AMRI amepata kura 26

Hivyo kwa matokeo hayo Mkurugenzi Mtendaji alimtangaza Mheshimiwa SWALEHE F. AMRI kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri.

**WAJUMBE WANNE WATAKAOUNGANA NA WENYEVITI WA KAMATI YA FEDHA,UTAWALA NA MIPANGO:**

1. Mhe. Zakina A.Mduma
2. Mhe. Selemani A. Mtili
3. Mhe. Salehe M.Kamtwanje
4. Mhe. Maua A. Makubui.

Hivyo baada ya uchaguzi huo kamati ziliundwa kama ifuatavyo:

**KAMATI YA FEDHA,UTAWALA NA MIPANGO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Rashidi C. Ndembo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Swalehe F. Amri | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rashidi N. Nambomo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Shaibu R. Ngumbe | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Selemani Mtili | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zakina Mduma | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salehe M. Kamtwanje | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Maua Makubui | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Bakari C. Mniyopa | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Rashidi A. Akbar | Mjumbe |

**KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Shaibu R. Ngumbe | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Menus M. Likuku | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rashidi Lugomba | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Jamal J. Nandonde | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hanafi N. Nahonyo | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zaituni L. Nawanda | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Arabia Mkwatile | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Hashimu B. Namawa | Mjumbe |

**KAMATI YA ELIMU AFYA NA MAJI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Rashidi N. Nambomo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Fabian J. Mahanyuka | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Saidi Mawangwa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Yahaya Lisinge | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hadija Likwembe | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rashidi B. Songoni | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Raia R. Nang'oko | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Zainabu Mpita | Mjumbe |

Kamati hii ya Elimu,Afya na Maji itaongozwa kwa awamu. Kwa sasa mwenyekiti ni Mhe. Rashidi N. Nambomo na baada ya miezi sita Kamati itaongozwa na Mhe. Rashidi Songoni hii imetokana na wakati wa uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kamati kura za wagombea kulingana.

**KAMATI YA MAADILI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Bakari C. Mnlyopa | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Athumani Mnlwasa | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Selemani Hiyari | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mohamedi Munga | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Simon Nachingulu | Mjumbe |

**KAMATI YA UKIMWI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Swalehe F. Amri | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Amina Mkanangwamba | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Sauda R. Rashidi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mohamedi Mnyolokoto | Mjumbe |

**MUHTASARI NA 18/2016/2017: KUFUNGA MKUTANO**

Mkurugenzi Mtendaji aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio na ushiriki mzuri katika Baraza la mwisho kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Alisisitiza kuongeza ushirirkiano kwenye shughuli zote za Halmashauri hasa kwenye usimamizi wa mapato ili kuweza kufikia malengo.

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe na wageni waalikwa kwenye Mkutano wa robo ya nne kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kusema kuwa ushirikiano ulioneshwa kwa mwaka mzima ni mzuri hivyo aliomba kuendelea na ushirikiano huo. Aliwapongeza Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine waliyochaguliwa kwenye kamati mbalimbali na kuwataka kushirikiana kama ilivyokuwa kwenye kamati za mwaka wa fedha 2016/2017. Mwenyekiti alifunga mkutano saa 10 : 50 jioni.

**"UMETHIBITISHWA"**

| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
|---|---|
| **JINA**....CHIWANGA R. NDEMBO.... | **JINA**....ROSSA M. CHITAE.... |
| **SAINI**....[signature].... | **SAINI**....[signature].... |

**SAINI**....02/11/2017....